BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 23 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2026/2027.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

191. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na ongezeko la taasisi, jumuiya, oganaizesheni mbalimbali ndani ya nchi yetu zinazohusika na masuala ya kijamii katika kutatua changamoto ndogo ndogo kwa wananchi. Taasisi hizi zinakabiliwa na changamoto nyingi bila ya kupata msaada wa kutosha kutoka Serikalini.

(a) Ni lini Serikal itazifanya taasisi, jumuiya na organaizesheni kuwa na uhuru mpana wa kufanya kazi kwa kuwawezesha pale wanapohitaji msaada.

(b) Ni lini Serikali itazisaidia taasisi hizi kuweza kunufaika na misamaha ya kodi kwa vitu vinavyoingizwa nchini kwa ajili ya misaada kwa jamii.

279. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika miradi ya ujenzi wa masoko inayoendelea kwa sasa;

(a) Je, Serikali inazingatia kikamilifu mahitaji ya wafanyabiashara na wananchi wanaotumia masoko hayo.

(b) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa na Serikali kuhakikisha masoko hayo yanakuwa na miundombinu bora, salama na rafiki kwa biashara pamoja na urahisi wa kupatikana bidhaa kwa wananchi.

<u>**Wizara ya Fedha na Mipango:**</u>

124. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Serikali ya Awamu ya Nane inafanya kazi kubwa na nzuri ya kutengeneza miundombinu ya barabara kila kona ya nchi hii. Hata hivyo, yapo maeneo ambayo barabara hizo zimetanuliwa na kuwafikia wananchi ambao wapo nje ya vipimo halisi vya barabaraba vilivyowekwa na sheria na walitakiwa walipwe fidia kwa thamani halisi ya ardhi na nyumba zao lakini utaratibu huo unaonekana haufanyiki na kuzusha malalamiko kwa waathirika.

(a) Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imeweka sharti la mali ya mtu kuchukuliwa na kulipwa fidia inayolingana na thamani ya mali hayo, kama ilivyo kwa kifungu cha 17(c), kwa nini sharti hili la Katiba halifuatwi kikamilifu kwa waathirika kama hao.

(b) Kwa nini kusianzishwe chombo huru cha kupitisha fidia stahiki kwa wananchi ambacho kitakuwa na utaratibu wa rufaa kama mtu hajaridhika ili kutekeleza kwa vitendo masharti ya kifungu cha 17(c) cha Katiba ya Zanzibar.

458. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuwa asilimia kubwa ya wakaazi wa Zanzibar ni waumini wa dini ya Kiislamu.

Ni kwa kiasi gani Serikali imejipanga kuimarisha huduma za kifedha kwa kutumia Mfumo wa Uchumi wa Kiislamu.

**<u>Wizara ya Kazi na Uwekezaji:</u>**

188. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Juhudi za kuwavutia wawekezaji haziwezi kwenda mbele na kuwa na mafanikio chanya bila ya kuwepo kwa rasilimali watu wa uhakika ambao watatumika katika utekelezaji wa miradi hiyo na kushirikiana na wawekezaji katika kufikia malengo.

(a) Ni lini Serikali itaona haja ya kuandaa Mfumo Maalum (Data base) kwa vijana wa kizanzibari pamoja na wasifu wao (CV) ili kuweza kupata nafasi katika miradi ya uwekezaji hapa nchini.

(b) Kwa namna gani Serikali inawasaidia wawekezaji wa ndani (Local Investors) kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

(c) Ni ipi ahadi ya Serikali kwa Wazanzibari katika kunufaika na uwekezaji unaoendelea hapa nchini.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

255. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni upi mpango wa Serikali wa kuongeza ubora wa skuli zake ili ziweze kushindana na skuli binafsi kutokana na kuwepo kwa tofauti kubwa ya ufaulu baina ya skuli hizi.

391. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Walimu wanaoshiriki kusimamia, kutunga na kusahihisha mitihani hawapati posho au posho hizo ni ndogo na hazijabadilika kwa muda mrefu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza au kurekebisha posho za mitihani ambazo hazijabadilika kwa zaidi ya miaka saba sasa.

(b) Kwa nini baadhi ya walimu wanaambiwa kuwa kazi hiyo ni sehemu ya majukumu yao na hawalipwi posho ilhali wengine hulipwa.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

2. MHESHIMIWA AZA JANUARY JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa kubinafsisha huduma za afya katika hospitali zetu za Unguja na Pemba.

(a) Je, Serikali imeshaifanyia tathmini Kampuni ya Saifee juu ya uendeshaji na utoaji wa huduma bora za kiafya katika hospitali zetu.

(b) Je, Kampuni ya Saifee imepewa muda gani wa kutoa huduma za afya hapa visiwani.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

434. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kuna pembejeo ambazo zinatolewa kwa wakulima ikiwemo mbolea.

Je, Serikali inaikagua mbolea ambayo inawapelekea wananchi wake ili kuepusha madhara ya mazao yao.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

113. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika eneo la Wilaya ya Kaskazini “A” Unguja kumekuwa na harakati za kuchimba mchanga ambazo zinaonekana kufanyika kinyume na utaratibu wa kukata vibali. Aidha, kumeonekana baadhi ya gari zinazobeba mchanga hazina hata namba na askari wanapowasimamisha hawasimami na baadhi ya wakati wanaposimama na kuulizwa kuhusiana na namba hudai jambo hilo

washughulikie wakubwa.

(a) Kwa sababu zipi Wizara haiifahamu changamoto hiyo ya kuchimbwa mchanga katika maeneo hayo bila ya kufuata utaratibu.

(b) Je, pamoja na kuwa hali hiyo inaendelea kwa muda mrefu kwa nini hakuonekani hatua zozote zinazochukuliwa kudhibiti.

119. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa hivi sasa kumeonekana hali isiyotabirika ya kupanda kwa bei ya nishati ya mafuta katika soko la ulimwengu ambayo pia inaathiri katika nchi zetu. Na kwa kuwa upandaji huo unaleta athari ya moja kwa moja ya mfumko wa bei ya bidhaa na huduma.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika kukabiliana na hali kama hiyo kila inapojitokeza.

(b) Je, nchi yetu imejiwekea utaratibu gani wa kuwa na akiba yake ya mafuta ili kupita salama katika vipindi vya changamoto za upandaji wa bei na upatikanaji wake kwa ujumla.

**<u>Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:</u>**

247. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Miongozo ya Wizara imezitaka taasisi zote za Serikali kutumia data center za Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) kwa lengo la kuhifadhi, kutunza taarifa za mifumo ya Serikali na kuongeza ufanisi lakini pia, kuimarisha usalama wa mtandao na mifumo ya Serikali. Hata hivyo, baadhi ya mifumo ya Serikali imekumbana na changamoto za kukosekana hewani kwa hitilafu ya undeshaji wa *Data center* hizo.

(a) Je, ZICTIA haina *Disaster Recovery Plan* wala *Backups Server* za kuaminika.

(b) Kwa nini ZICTIA haina *reliable backup power* za kuendesha *data center.*

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

155. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Baadhi ya gari kimtazamo zinaonesha kuwa ni mbovu lakini bado zinazoendelea kutumika barabarani na kuhatarisha maisha ya wananchi.

Je, Serikali inadhibiti vipi gari hizo ili zisiendelee kuleta athari kwa wananchi.

294. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa ujenzi wa barabara unaendelea hapa nchini kupitia kampuni tofauti kwa kiwango kikubwa sana. Ujenzi huo unatumia rasilimali zisizorejesheka zinazochimbwa hapa nchini ikiwa ni pamoja na mawe, fusi na mchanga.

Je, kuna makubaliano gani ya kisheria baina ya Serikali na Kampuni hizo za ujenzi kwa kutumia rasilimali zetu za maliasili zisizorejesheka katika ujenzi wa miundombinu ya hapa nchini.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

187. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Sekta ya Utalii ndio uti wa mgongo wa uchumi katika jamii na nchi kwa ujumla. Hata hivyo, sekta hii kwa sasa imekosa usimamizi madhubuti na sheria katika utekelezaji wake hali inayosababisha kudumaa kwa utalii wetu ndani ya visiwa vya Zanzibar.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kudhibiti watoa huduma binafsi za waongoza wageni (Tour Guide) ndani ya hoteli kubwa ili fursa ziwe za kuwanufaisha wazawa wa Zanzibar moja kwa moja.

(b) Ni juhudi zipi za makusudi inazochukua Serikali katika kuutangaza utalii kimataifa ili kuongeza hadhi ya utalii wetu.

(c) Ni upi mpango wa Serikali wa kuwezesha kukifungua kisiwa cha Pemba ili kuongeza idadi ya watalii.

396. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Mnamo siku ya tarehe 11/4/2026, majira ya saa 11:00 za jioni Askari wa Mamlaka ya Mji Mkongwe wakiongozwa na gari ya Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo walifika eneo la Darajani na kuwavamia baadhi ya wafanyabiashara kwenye eneo moja na kutaka kuchukuwa vitu vyao. Aidha, katika eneo hilo karibu na "Youth League" walikuwepo wafanyabiashara wengine ambao hawakuguswa hali ambayo inaonekana hatua zinachukuliwa kwa ubaguzi kinyume na kifungu cha 12(4) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinachokataza ubaguzi.

(a) Je, sababu gani zinafanya Mamlaka ichukuwe hatua kali tofauti kwa wafanyabiashara katika eneo moja kwa maana wengine kuwakamata na wengine hapo hapo hawaguswi.

(b) Je, vitu vya wafanyabiashara vinavyochukuliwa na askari vinapelekwa wapi wakati wenyewe wanakuwa hawachukuliwi.

(c) Je, kuna utaratibu gani unaofanyika wa kuwarejeshea wenyewe vitu vyao na kuwaondolea hasara kwa kuwa vitu hivyo hununuliwa kwa pesa za mitaji midogo midogo na wengine wanakopa.

<u>**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**</u>

260. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa vijana waliopo kisiwani Pemba na hasa katika jimbo la Mkoani wanapatiwa mikopo kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (2025-2030).

## III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:**</u>

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2026/2027.

**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2026/2027.

Zanzibar,
23 Mei, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR